Wataalamu wa Vikwazo
Walimu wa Utiifu

Shirika la Kimataifa la Uhodari
wa Uwezo & Utiifu, LLC

24 Septemba 2018

Vikwazo vya Umoja wa Mataifa
Mamlaka za Udhibiti wa Mipaka ya Afrika

Imetayarishwa na Thomas Bifwoli

Utangulizi

Maafisa wa ushuru na ulinzi wa mipaka wako kwenye safu ya mbele ya kila nchi ya kulinda dhidi ya biashara haramu inayovuka mipaka, ikiwemo ile inayohusu vikwazo vya Umoja wa Mataifa na marufuku ya silaha na bidhaa za kijeshi za Korea Kaskazini. Hata hivyo, mamlaka za ushuru barani Afrika zimeonekana kuwa zinaupatia kipaumbele ukusanyaji wa mapato kuliko usalama wa mipaka. Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki za Kenya, Uganda, Tanzania, Rwanda, na Burundi zote zina majukumu yao husika ya kukusanya mapato (Ushuru na Mapato ya Ndani ya Nchi) chini ya wakala moja.[1] Uhamasishaji wa mapato ya ndani ya nchi unategemea ukuaji wa uchumi wa nchi husika za EAC. Hii pia ndio hali ndani ya nchi nyingi barani Afrika. Mfano ni Mamlaka ya Ukusanyaji wa Ushuru na Mapato ya Uhabeshi ambayo ina jukumu la kukusanya ushuru na kodi za ndani ya nchi. Tatizo ni kuwa uchumi wa nchi hizi unaendeshwa ndani ya mazingira tofauti ya uendeshaji. Baadhi ya nchi za EAC, kama vile uchumi wa nchi nyingi barani Afrika, zinaathiriwa na, miongoni mwa mengine, vita vya wenyewe kwa wenyewe vya ndani, maongezeko ya bei yasiyodhibitiwa, na kupanda na kushuka sana mno kwa viwango vya ubadilishaji wa sarafu zinazoweza kuathiri sana mapato ya ndani ya nchi.

Kwenye mwaka wa kifedha wa 2014/2015, Mamlaka zote za Ukusanyaji wa Mapato (RA) ndani ya eneo la EAC zimerepoti kuwa ukusanyaji wa mapato umeongezeka kimarudufu ukilinganishwa na miaka iliyopita, kama ifuatavyo: OBR (Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato Nchini Burundi) Milioni 415.45, RRA (Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato Nchini Rwanda) Milioni 1,230.90, KRA (Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato Nchini Kenya) Milioni 11,713.64, TRA (Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato Nchini Tanzania) Milioni 6,059.80, na URA (Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato Nchini Uganda) Milioni 3,371.03. Licha ya ukusanyaji wa mapato ulioongezeka kwenye Mamlaka zote za Ukusanyaji wa Mapato, Mamlaka za Ukusanyaji wa Mapato Nchini Burundi na Uganda tu zimepitisha shabaha zao kwa kufikisha asilimia 117.2 na 101.4% kwa mtawalia. Mamlaka zilizobakia hazikufikisha shabaha zao.[2]

[1] Kiasili, lengo kuu la kila Mwanachama wa EAC limekuwa ukusanyaji wa mapato.
[2] Kulingana na ripoti ya Uchambuzi wa Kilinganizi wa Mamlaka za Mapato za Afrika Mashariki ya 2014/2015 iliyochapishwa mnamo 2016.

Rico Carisch
rico.carisch@comcapint.com
+1-610-390-9541

www.comcapint.com
110 West 94 Street – 2D
New York, NY 10025

Loraine Rickard-Martin
loraine.rickard-martin@comcapint.com
+1-917-715-2142

Mbali na changamoto inayokumba ukusanyaji wa mapato, ufuatilizi wa mizigo iliyoko njiani inayoenda kwenye nchi ambazo hazina bandari pia ni changamoto inayokumba nchi nyingi na mamlaka zao za ushuru. Japokuwa nchi hizi zinasisitiza ukusanyaji wa mapato, data inayopatikana inaonyesha ongezeko la mizigo iliyoko njiani ambayo kimsingi haitozwi kodi kwenye sehemu ya kwanza ya kuingia. Kwenye hali murwa kabisa, kunafaa kuwekwe mifumo ya kuhakikisha kuwa mizigo iliyoko njiani haiendi kwenye soko la kienyeji. Kwa ziada, kusisitiza kidogo mizigo iliyoko njiani pia inamaanisha kuwa bidhaa zinazohusishwa kwenye vikwazo vya Umoja wa Mataifa zinaweza kuepuka kirahisi ufuatilizi wa mamlaka ya ushuru. Hapo chini, angalia mfano wa mizigo iliyoko njiani inayopitia bandari ya Mombasa.

Jedwali: Mizigo Iliyoko Njiani inayopitia bandari ya Mombasa[3]			
Nchi ya kuwasili	Mwaka wa 2017 (Kwa Tani)	Mwaka wa 2016 (Kwa Tani)	% ya mgao wa Kuwa Njiani
Uganda	7.112.971	6.346.715	82.3%
Sudani Kusini	673.752	597.852	7,8%
Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo	360.124	376.935	4,2

Haja inayoendelea kuongezeka ya kusaidia biashara na kukusanya mapato inayokumba mamlaka za ushuru inaleta changamoto kwenye usimamizi wa vikwazo vya Umoja wa Mataifa. Kuna ushahidi kidogo sana wa ufuatilizi unaozaa matunda wa vitisho vingine vya kimataifa vikiwemo ugaidi ambayo ni miongoni mwa majukumu ya kimataifa ya nchi ambazo ni wanachama.

Ukusanyaji wa Mapato dhidi ya Udhibiti wa Mipaka

Kwenye uchumi wa nchi zinazotegemea ukusanyaji wa mapato kutoka kwa utozaji Ushuru, ukusanyaji wa mapato imepatiwa kipaumbele na mamlaka za Ushuru. Hii ndio hali iliyoko zaidi kwenye nchi zinazostawi. Kwa upande mwingine, mataifa yaliyoendelea yanasisitiza zaidi usalama wa mipaka haswa kwenye utoaji na uingizaji wa vikatazwavyo na vizuiwavyo.[4] Kwenye EU, kwa mfano, bidhaa zinaweza kuhamishwa bila pingamizi kwa kuvuka mipaka ya nchi na kwa ajili ya haya, mapato ya kiwango cha chini yanakusanywa na mawakala ya ushuru kwenye nchi husika. Mwelekeo wa hivi karibuni wa biashara huru ulimwenguni na kuongezeka kwa tishio la Ugaidi wa kimataifa umesababisha usalama wa mipaka upewe kipaumbele kwenye uchumi wa nchi nyingi. Muungano wa ushuru ulibuniwa kwenye jumuiya ya EAC

[3] Chanzo: Data ya huduma za shirika la Mamlaka ya Bandari Nchini Kenya.

[4] David Widdowson; Shughuli inayobadilika ya ushuru; maendeleo au mapinduzi. Jarida la Ushuru Ulimwenguni, Buku la 1, nambari ya 1 ukurasa wa 31

(ukaanzilishwa upya na mkataba wa 1999[5]), na kuna kiwango kiasi cha uhamishaji huru wa bidhaa kwenye kundi hili la eneo la biashara, haswa pamoja na uanzilishaji wa eneo moja la ushuru mnamo 2013.[6] Hata hivyo, lengo kuu la kuwepo kwa mamlaka za ushuru ni kukusanya mapato. Makubaliano kama hayo ya biashara ya kieneo yametiwa saini. Kwa mfano, Biashara ya Uvukaji Mipaka Isiyo Rasmi (ICBT) na Utawala wa Usalama wa Uvukaji Mipaka (CBSG) zilitiwa saini mnamo Juni 2018 na nchi za eneo la Mamlaka Baina ya Serikali inayohusu Maendeleo (IGAD).[7] Mpango huu unalengwa kuleta usimamizi bora zaidi wa biashara ya uvukaji mipaka miongoni mwa nchi za IGAD

Licha ya juhudi za kuongeza mgawo wa kodi za ndani ya nchi zilizofanywa na Mamlaka za Ukusanyaji wa Mapato za EAC, mchango wa utozaji ushuru kwenye mapato ya jumla ya kodi umeendelea kuwa chanzo kikuu cha mapato. Hii haiangazii nia ya serikali za kundi la eneo la EAC ambayo ni kurahisisha mwingiliano wa biashara wa kieneo na kiulimwengu. Nchi hizi zimeendelea kutegemea utozaji ushuru kwa ajili ya msingi mwembamba wa kodi za ndani ya nchi. Hii imesababishwa sana na uchumi wa pesa na sekta kubwa ambayo si rasmi ambazo zinaleta changamoto ya kukidhi shabaha za ukusanyaji wa mapato.

Takwimu za kulinganisha (ukusanyaji wa ushuru) za mamlaka husika za ukusanyaji wa mapato ni kama zifuatazo: Kwa miaka miwili ya 2014/15, Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato Nchini Uganda (URA) ilidumisha mgawo wa Ushuru wa asilimia 42%, ambao ni kama wa 2013/14, huku punguzo dogo la mgawo wa kodi za biashara ya kimataifa lilionekana kwenye Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato Nchini Kenya (KRA), ambayo ilirekodi asilimia 32.5% ikilinganishwa na asilimia 33.3% mnamo 2013/14; Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato Nchini Rwanda (RRA) ilipata asilimia 30.8% mnamo 2014/15 ikilinganishwa na asilimia 31.7% kwenye mwaka uliopita, na Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato Nchini Burundi (OBR) ilirekodi asilimia 34.7% mnamo 2014/15 kutoka asilimia 37.0% iliyorekodiwa mnamo 2013/14. Mgawo wa ushuru ukilinganishwa na mapato yote ya kodi ya Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato Nchini Tanzania (TRA) uliongezeka kwa kurekodi asilimia 38.8 juu zaidi ikilinganishwa na asilimia 36.7 mnamo 2013/14.

Yaliyopo hapo juu yanaonyesha umuhimu wa idara za ushuru na kazi yao ya ukusanyaji wa mapato kwenye nchi za EAC. Kwa mfano, nchini Kenya, mafunzo yaliyopewa maafisa wa ushuru yana lengo kuu la kuboresha ukusanyaji wa mapato. Hali nyingi zimetambuliwa ambapo maafisa hata hawajui vikwazo vya Umoja wa Mataifa vyenye nguvu za kisheria na hawana uwezo wa kutambua matukio ya biashara haramu. Hivi karibuni, kumekuwa na msisitizo kubwa wa kufanya huduma za ushuru ziwe otomatiki kwenye nchi anuwai barani Afrika ambao

[5] EAC ilianzishwa mnamo 1967, ilivunjwa mnamo 1977 na ilifufushwa mnamo 1999. Soko la pamoja, muungano wa ushuru, muungano wa sarafu, na mashirikisho ya kisiasa, ni nguzo kuu za mkataba wa hivi karibuni.

[6] Eneo Moja la Ushuru (SCT) lililorudishwa na "washiriki wanaolitaka – "kiasili Kenya, Uganda na Rwanda, na baadaye, Burundi na Tanzania -- lilikuwa na nia ya kuharakisha utekelezaji wa Muungano wa Ushuru uliotarajiwa kwenye Mkataba wa EAC mnamo 1999.

[7] Nchi za IGAD zinajumuisha Kenya, Jibuti, Eritrea, Uhabeshi, Sudani, Sudani Kusini, Uganda na Somalia.

Enrico Carisch
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

www.comcapint.com
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025

Loraine Rickard-Martin
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

unalenga kukuza biashara na kufunga vipenyo vya kupoteza mapato badili ya kulenga usalama wa mipaka. Haya yanajumuisha kuleta mifumo ya kuendesha sambamba na kuongeza uzalishaji wa taratibu za ushuru, kupunguza ufisadi, na kuboresha mbinu za kuwekea thamani ambazo zinaweza kuongeza mapato ya serikali. Mifumo hii inasisitiza kidogo sana kupunguza usafirishaji haramu na kuzuia uhamishaji unaovuka mipaka wa bidhaa haramu/zilizokatazwa.

Ni lazima Mamlaka za ushuru barani Afrika ziunde vifaa na miradi ya jumla ili kukuza mifumo ya haraka na yenye ufanisi ya udhibiti yanayolenga kuzuia biashara haramu zinazofanywa na nchi zilizowekewa vikwazo vya Umoja wa Mataifa kwenye viwango vya kitaifa na kieneo. Muungano wa Afrika umejaribu mara kadhaa kuzisaidia nchi ambazo ni wanachama ziendeleze sera na miongozo inayoweza kuwezesha nchi hizi kudhibiti mipaka yao vizuri zaidi.[8] Hakuna ushahidi ulioko kwenye utafiti wa kina unaoonyesha kufaulu kwa juhudi hizi. Kile kilicho wazi ni kuwa nchi nyingi bado zinakumbana na changamoto kwenye udhibiti wa mipaka yao kama inavyoonyeshwa na utafiti anuwai ukijumuisha ripoti za wataalamu wa jopo la Umoja wa Mataifa linaloangazia Korea Kaskazini. Limepata mifano mengi ya biashara baina ya nchi fulani na Korea Kaskazini ambayo mara nyingi inajumuisha bidhaa za kijeshi zisizoruhusiwa zinazoingia nchi za Afrika, huku bidhaa ambazo zimewekewa vizuizi zinapelekwa Korea Kaskazini.

Mojawapo ya sababu za kushindwa kufaulu kwa utiifu wa vikwazo ni mashirika ya udhibiti wa mipaka barani Afrika kulenga tu kuongeza ukusanyaji wa mapato. Hata pamoja na malengo haya, nchi za EAC zinakumbana na changamoto za kukidhi shabaha zilizowekwa za mapato, kama ifuatavyo:

1. Kulingana na ripoti ya halmashauri ya kiufundi ya Mamlaka za Ukusanyaji wa Mapato za Afrika Mashariki ya 2016, ilitambuliwa kuwa miongoni mwa changamoto zinazokumbwa na mamlaka za ukusanyaji wa mapato ni jinsi ya kushughulikia sekta isiyo rasmi inayoendelea kukua. Ukuaji huu, kwenye hali murwa, unafaa ugeuke uwe msingi uliongezeka wa kodi na, kutokana na haya, mapato zaidi yanafaa kukusanywa. Hata hivyo, changamoto zilizoko kwenye sekta ni za kimsingi kama vile ukosefu wa uhodari wa usimamizi wa kifedha na uhasibu, na wahusika kuhama mara kwa mara kutoka kwa sekta moja hadi nyingine. Mamlaka nyingi za Ukusanyaji wa Mapato hazina vifaa vya kushugulikia changamoto hizi.

2. Changamoto ya pili ni kujenga uwezo. Kwenye ripoti hiyo hiyo (EACRATC ya 2016) ilitambuliwa kuwa kujenga uwezo ilikuwa changamoto kwenye Mamlaka zote za EAC za Ukusanyaji wa Mapato. Kwenye OBR, kwa mfano, iliripotiwa kuwa wafanyikazi wengi wapya walihitaji mafunzo ya kudumu; lakini hakukuwa na rasilimali za kuwafunza maafisa hawa. Kwenye Mamlaka zingine za Ukusanyaji wa Mapato, kwa mfano TRA, iliripotiwa kuwa maafisa wana ukosefu wa uhodari wa

[8] Angalia nyongeza za jitihada za kieneo zilizofanywa na Muungano wa Afrika.

kimsingi wa kukagua walipaji kodi na, kwa ziada, wana ukosefu wa elimu ya sekta maalum kama vile “mawasiliano ya anga, huduma za fedha, mafuta, gesi, uchimbaji madini, na utalii”.

3. Tatu, kuna kukawia kwenye kukubaliwa kwa sera ya kodi na/au elimu ndogo ya kile kinachohitajika kuboresha sera husika ili kusaidia Mamlaka za Ukusanyaji wa Mapato zikidhi lengo lao la kimsingi, yaani, ukusanyaji wa mapato. Kwenye Mamlaka zote za Ukusanyaji wa Mapato za EAC, ilionekeana (ripoti ya EACRATC) kuwa baadhi ya sera husika zilikawia bila kuhitajika, au zilikataliwa kabisa, na kusababisha athari mbaya kwenye malengo ya ukusanyaji wa mapato.

Mabadiliko Yaliyoshughulikiwa na Changamoto ya Udhibiti wa Mipaka

Afrika ina mipaka 109 ya kimataifa yenye urefu wa jumla wa takriban kilomita 45,000. Kati ya mipaka hii, chini ya asilimia 35% yamewekewa vikomo kwa uwazi. Mipaka ya Afrika yana sifa za kiwango cha juu cha uvujaji na usimamizi mbaya.[9] Hali hii inatoa fursa kwa aina zote za shughuli za kihalifu za uvukaji mipaka zipate kutokea. Pia inaitisha mabadiliko kwenye mikakati ya nchi za Afrika, kwani kulinda mipaka ni jukumu la kimsingi la nchi binafsi.

Juhudi nyingi zimefanywa ili kushughulikia changamoto zinazokumba Mamlaka za Ukusanyaji wa Mapato zikiwemo kufanya otomatiki taratibu zao, lakini ni dhahiri kuwa mambo mengi zaidi yanahitaji kufanywa ili Mamlaka hizi za Ukusanyaji wa Mapato ziweze kushughulikia changamoto nyingi zinazokumba mamlaka hizo. Kama ilivyoelezwa hapo juu, nchi nyingi barani Afrika zinapoendelea kusisitiza ukusanyaji wa mapato, bado zinakumbana na changamoto za kukidhi shabaha za mapato na pia kushughulikia changamoto zingine husika za kudhibiti mipaka na usalama. Kwa ziada, kumekuwa na ufaulu wa kiwango cha chini kwenye uratibu na uoanishaji wa juhudi za usimamizi wa mipaka kwenye nchi nyingi barani Afrika.[10]

Hapo chini, kuna uangalizi wa changamoto za kimsingi za kudhibiti mipaka ambazo zikishughulikiwa, zitasaidia sana nchi za Afrika: 1) Kufikia shabaha za mapato; na 2) Kushughulikia changamoto za usalama wa mipaka zikiwemo utekelezaji wa vikwazo husika vya Umoja wa Mataifa.

Matatizo/Changamoto kwenye Utekelezaji Sheria Mipakani na Suluhu Ziwezekanazo

Matatizo yaliyotambuliwa hapo chini mara nyingi yanaathiri nchi za Afrika ingawa pia yanaweza kuwepo kwenye nchi zingine zinazostawi. Hizi ni, miongoni mwa zingine, changamoto za kimsingi zinazoathiri ufuatilizi wa vikwazo wenye ufanisi.

[9] Mradi wa Mipaka wa Muungano wa Afrika Addis Ababa, 2012
[10] Ibid

1. **Ukosefu wa mifumo ya utekelezaji sheria mipakani na miundombinu dhaifu (barabara n.k.)**

Kwenye nchi nyingi barani Afrika, mipaka na maeneo makubwa yako kwenye maeneo yaliyoko mashinani na yenye idadi ndogo sana ya watu, kwa hivyo, hii inafanya shughuli za utekelezaji sheria ziwe ngumu sana kufanya kwa njia ya ufanisi. Kwenye nchi hizi, usalama wa mipaka na utekelezaji sheria mipakani unalengwa haswa kwenye poti za kuingia na sehemu zingine kuu za kuingia. Sehemu ndogo zaidi za kuingia hazishughulikiwi, na mara nyingi, zinatumiwa kwa bidhaa haramu na bidhaa zilizopigwa marufuku. Kwa ziada, maafisa wa mipaka na ushuru mara nyingi hawana rasilimali za kutosha za kusimamia maeneo haya kama inavyotakikana; hii inarahisisha uhamishaji haramu wa mizigo wa uvukaji mipaka.

Kuna sehemu nyingi za kuvuka zinazojulikana, za haramu na zisizo rasmi, ambazo hazidhibitiwi wala hazifuatiliwi vizuri. Kwa mfano, kuna barabara kadhaa zinazovuka mipaka ambayo hayana vitengo/ofisi/vituo vya mamlaka ya ushuru au ambayo yana vitengo/ofisi/vituo kidogo vya mamlaka ya ushuru. Ushikaji doria mipakani na baina ya vituo vya mipaka si wa mara kwa mara, ni wa kiasi kidogo na unapewa kiwango kidogo cha rasilimali. Mifumo iliyopo inatoa upinzani usiotosha kwa matembezi huru ya watu na bidhaa haramu.

Vituo vyingi vya mipaka vilivyoko mashinani vina wafanyikazi kidogo na baadhi ya vituo hivyo vina ukosefu wa rasilimali za bidhaa za kimsingi zinazohitajika kwenye ulinzi wa sheria mipakani unaozaa matunda, kama vile kompyuta, Intaneti, nguvu za umeme za kudumu, sehemu zinazofaa za kuishi maafisa wa mipaka, magari, na vituo vinavyofaa vya kuhifadhi na kutafuta.

Miundombinu yanayofaa kama vile vifaa vya ugunduzi na skana hayapatikani kwenye vituo vingi vya mipaka barani Afrika, ambayo inatoa fursa kwa usafirishaji haramu kwani ni taabu kugundua bidhaa haramu. Kuwepo kwa maeneo haya mashinani kunawezesha ufikiaji mdogo wa maelezo kwa muda halisi ili kusaidia juhudi za utekelezaji.

2. **Upungufu wa wafanyikazi na mafunzo dhaifu**

Inayohusu kidokezo cha 1 hapo juu ni idadi isiyotosha ya wafanyikazi wa kuhimili shughuli kubwa, zikiwemo kushika doria ambako kunazaa matunda. Hata mizigo ikizuiliwa, hali hizi zinaweza kuchangia usahihi uliopungua kwenye uthibitishaji. Tatizo linazidishwa na udhaifu wa kufanya taratibu ziwe otomatiki ambao unasababisha kazi nyingi zifanywe kimkono. Waajiriwa wa usalama wa mipaka ya nchi mara nyingi huwa ni kidogo mno, hawajapewa mafunzo ya kutosha na hawajapewa vifaa vya kutosha kulingana na kiwango cha changamoto wanazokumbana nazo na, kwa ajili ya kuwepo mashinani kwa maeneo mengi ambao wanafanya kazi, wana wajibu wa viwango vya chini wa matendo yao.

Enrico Carisch
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

www.comcapint.com
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025

Loraine Rickard-Martin
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

Maajenti wa mipaka walioidhinishwa kusimamia mipaka ya nchi hawana uwezo wa kufanya majukumu yao kwa ufanisi. Hali hii iko kwenye nchi nyingi. Hali hii ni mbaya zaidi kwenye nchi zenye vita kama vile Sudani Kusini, miongoni mwa nchi zingine. Ukosefu wa nafasi ya ofisi na ukosefu wa makaazi ya waajiriwa wa kudhibiti na kushika doria mipakani, pamoja na mbinu za mawasiliano zisizotosha pia zimejaribu sana uwezo wa maajenti hawa wa kufanya kazi zao vizuri. Kwa ziada, uhodari usiotosha na uelewaji dhaifu wa kazi upo sana. Yanayozidisha matatizo haya ni ujulikanaji dhaifu wa sheria za ushuru, makubaliano ya kieneo na makubaliano ya kimataifa ya biashara, kwa mfano, vikwazo, ambazo zinahusu utenda kazi mzuri wa kazi zao.

Kozi fupi za ugeuzaji zinazopewa wafanyikazi haziwapatii ujuzi unaohitajika wa kufanya kazi kwenye idara za ushuru. Kwenye mojawapo ya nchi ambayo ni mwanachama wa EAC kwa mfano, tukio limetajwa ambapo afisa wa ushuru alishindwa kufanya hesabu ya kupata thamani ya ushuru (mara nyingi inajumuisha gharama, bima na mizigo). Kuna haja ya mafunzo ya kudumu ya waajiriwa wa mipaka. Mafunzo fulani ni lazima yajumuishe kuajiri na kuwashughulikia wanaotoa taarifa za siri, mbinu za utafutaji, mbinu za uangalizi na ukusanyaji wa maelezo, na uelewaji na ufasiri wa mienendo na takwimu za uhalifu

Wafanyikazi wote kutumia vifaa maalum kwenye vituo vya mipaka inafaa kutumika kote Uhodari wa kompyuta na uwezo wa wafanyikazi wote kufikia shughuli zote zinazopatikana kwenye mtandao wa kompyuta zitasaidia sana ugunduzi wa bidhaa haramu na bidhaa zisizoruhusiwa.

3. Kiwango duni cha kufanywa otomatiki

Mifumo ya ushuru iliyofanywa otomatiki inatoa kifaa muhimu cha kuongeza uwazi kwenye tathmini ya ushuru na kodi, kupunguza kimarudufu muda wa kumaliza taratibu za ushuru, na kugundua bidhaa haramu/zisizoruhusiwa. Inajulikana kuwa kila kiwango cha kufanya otomatiki taratibu za ushuru kinapopanda nchini, ndipo kuna uwezekano mkubwa zaidi wa ukaguzi wa kina, ugunduzi wa udanganyifu, na hatua kali kama vile kufungulia mashtaka mahakamani.

Uanzilishaji wa teknolojia ya hivi sasa unafaa kupewa kipaumbele na serikali za Afrika ili kupambana na uhalifu wa uvukaji mipaka. Kwa ajili ya upana wa maeneo ya mipaka, ni lazima tuhusishe matumizi ya teknolojia iliyoimarishwa kama vile kamera, roboti, na skana, miongoni mwa zingine.

Mamlaka za ushuru kwenye nchi anuwai barani Afrika pia mara nyingi hazina hifadhidata za kitaifa za wahalifu, mitandao yao na aina na viwango vya bidhaa haramu zilizokamatwa.

Kuna haja ya kurekebisha taasisi, kupata na kutumia teknolojia zisizohitaji watu ili zifanye kazi pamoja na vidhibiti haswa vya mipaka, kutumia vizuri teknolojia, na kuendeleza mafunzo ya wafanyikazi kulingana na mahitaji ya sasa ya mipaka. Serikali barani Afrika zinafaa kutumia mifumo ya kina ya kukusanya maelezo kuhusu usafirishaji haramu ili kusaidia usambazaji wa

Enrico Carisch
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

www.comcapint.com
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025

Loraine Rickard-Martin
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

maelezo kuhusu mienendo, ruwaza na asili inayobadilika ya njia za usafirishaji haramu, na zinafaa kuunda hifadhidata kuhusu wanaosafirisha bidhaa haramu waliohukumiwa na kufungwa.

4. Kutokuwepo kwa serikali kwenye maeneo tata

Kwenye maeneo tata barani Afrika, hakuna watawala, au wapo lakini hawashughuliki. Utafiti wa udhibiti na usalama wa mipaka kwenye maeneo ya mpaka wa Liptako-Gourma baina ya Mali, Niger na Burkina Faso ulionyesha kuwa, licha ya kuwa serikali inaaminiwa sana, matatizo ya usalama kwanza yanashughulikiwa kwa kutumia mifumo ya jadi ya kutuliza migogoro, na watawala wanafuatwa kusipokuwa na budi. Hii inaonyesha kuwa serikali za nchi hizi haziwezi kudhibiti vizuri maeneo ya mipaka yaliyoko mashinani kwa kutumia jamii zinazoishi mipakani kushughulikia changamoto za uvukaji mipaka. Hii imechangia kwenye ongezeko la ulanguzi wa silaha na bidhaa haramu barani Afrika. Ugumu wa kushika doria mipakani pia umewezesha mashirika ya kigaidi yaweze kufanya shughuli zao kwa kuvuka mipaka kwa urahisi.

5. Ukosefu wa ushirikiano baina ya mawakala ya serikali

Kwenye kiwango cha serikali, mara nyingine kuna mwingiliano kidogo au hakuna mwingiliano kabisa baina ya idara tofauti kama vile uhamiaji, mamlaka za ushuru, polisi na vitengo vya upelelezi. Mojawapo ya shida kubwa kabisa ni ukosefu wa kugawiza upelelezi kuhusu uhalifu wa uvukaji mipaka miongoni mwa mawakala haya. Kutogawiza upelelezi wa uhalifu kuhusu magenge au makundi ya uhalifu ya kimafia miongoni mwa mawakala tofauti ya utekelezaji sheria kunapinga taratibu za kuingilia kati na kukamata bidhaa haramu na bidhaa zisizoruhusiwa. Mamlaka na mawakala yanayohusika kwenye udhibiti wa mipaka na ushuru ni lazima yafanye kazi pamoja ili kusuluhisha matatizo ya jumla, badili ya kufanya kazi kivyao na mara nyingi wakiwa na malengo yanayopingana.

Ushirikiano wa karibu baina ya mawakala ya serikali ni muhimu sana kwenye udhibiti mzuri wa mipaka. Wana masafa marefu sana wanayofaa kuyashughulikia lakini hawana watu wa kutosha kufanya hivyo, kwa hivyo, mawasliano mazuri na matumizi bora kabisa ya rasilimali zinazopatikana ni muhimu sana. Hii sio hali kwenye mipaka mengi barani Afrika. Ukosefu wa ushirikiano baina ya mamlaka unawekea kikomo tendo ambalo lingeweza kufanywa ili kuzuia uhalifu huu.

Serikali barani Afrika zinafaa kufanya kazi kwa karibu ili kukuza usalama wa mipaka kwa kugawiza maelezo ya upelelezi na kushika doria kwa pamoja mipakani. Kutokuwepo au ukosefu wa mashirika thabiti ya kusimamia mipaka pamoja na ukosefu wa ushirikiano na mwingiliano kwenye viwango vya kienyeji na kieneo unasababisha mipango isiyolingana ya mifumo ya usimamizi wa mipaka, na kuunda vipenyezo vya usafirishaji haramu na uhalifu mwingine wa mipaka.

Enrico Carisch
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

www.comcapint.com
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025

Loraine Rickard-Martin
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

Kuimarisha ushirikiano baina ya nchi barani Afrika na jamii ya kimataifa, haswa kwenye nyanja ya utekelezaji sheria, ugawizaji wa upelelezi na maelezo, mafunzo na mahojiano yanayodumishwa, yataendelea kukuza usalama wa mipaka.

6. Uhalifu wa kimafia

Uhalifu wa kimafia una mbinu nyingi, zikiwemo kuuza maelezo kwa makundi ya uhalifu, kusaidia kupita kwa bidhaa haramu na kupinga uchunguzi. Kuuza maelezo kunaweza kujumuisha kutoa maelezo kwa makundi ya uhalifu kuhusu uchunguzi unaoendelea au maelezo ya kitaratibu yanayosaidia makundi ya uhalifu kuepuka kugunduliwa.

Barani Afrika, usafirishaji wa bidhaa haramu ni miongoni mwa shughuli za uvukaji mipaka ambazo mara nyingi zinahusishwa na uhalifu wa kimafia. Kwenye baadhi ya hali, walinzi wa mipaka wenyewe wanaweza kuhusika kwenye shughuli za usafirishaji haramu. Makundi ya uhalifu yameonekana kuwa yanajaribu mno kutambua maafisa wanaoweza kuathiriwa ambao wana uwezekano mkubwa wa kutikia muamala wa ufisadi, au kuingilia mawakala ya ulinzi wa mipaka na utekelezaji sheria kwa kutumia hongo na vitisho. Maafisa wa ushuru pia wanaweza kutoa dhamira bandia kwa wahalifu wa kimafia kwa kuunda rekodi bandia au kuingiza maelezo bandia kwenye mfumo. Hati ambazo zinaweza kuundwa bandia zake ni orodha za bidhaa, vyeti vya asili na hati zingine za uletaji nchini.

Kwenye hali zingine, ambapo wafanyikazi wa kudhibiti mipaka wamekamata bidhaa haramu, wanaofanya usafirishaji haramu wanapanga njama na walioko serikalini ili kuvunja juhudi zao.

Hadi leo, hakuna data inayopatikana ambayo inaweza kukifanya wazi kiwango, kikiwa kipo, cha biashara isiyoruhusiwa inayofanywa na Korea Kaskazini inayojumuisha makundi ya uhalifu ya kimafia yanayofanya shughuli zao ndani ya Afrika Mashariki.

7. Ufisadi

Kwa ajili ya asili ya taratibu za ushuru, sheria za ushuru zinawapatia uamuzi mpana maafisa walioko kwenye safu za mbele. Utekelezaji wa uamuzi huu unakumbwa na matumizi mabaya ya mamlaka ambayo yanaweza kukuza ulanguzi haramu. Tukizingatia changamoto anuwai ambazo hata maafisa wa ushuru wenye nia nzuri wanakumbana nazo, maafisa hao wanaweza kupata shida ya kuzingatia kwa makini uletaji nchini wa bidhaa za kijeshi za Korea Kaskazini.

Mkusanyiko wa kulipwa kidogo, hali ngumu za kufanya kazi, na uwezekano mdogo wa kugunduliwa zinaleta mvutio na fursa za kuhongwa. Kwenye baadhi ya nchi barani Afrika, kwa sababu kiwango cha mshahara wa maafisa wa mipaka ya nchi ni chini ya kipato cha kuishi nchini, baadhi ya maafisa wanaitisha hongo ili kuongeza kipato chao. Kwa ziada, tofauti ya mshahara wa mlinzi wa mipaka au afisa wa ushuru na kipato anachoweza kupata kutokana na ufisadi daima itakuwa kubwa na ina uwezekano mkubwa wa kuzidisha ufisadi.

Enrico Carisch
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

www.comcapint.com
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025

Loraine Rickard-Martin
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

Ufisadi unafanya mipaka iweze kuzidi kuathiriwa na vitisho kama vile ulanguzi wa watu, madawa ya kulevya, bunduki ndogo na silaha hafifu, na pia matukio ya hivi karibuni ya ugaidi. Yanayozidisha tatizo ni mawakala yasiyokuwa na wafanyikazi wa kutosha na wafanyikazi wasiokuwa na ari ambao hawashirikiani na hawaratibu shughuli zao za kitaifa na kieneo huku wakijiburudisha na nguvu pana za uamuzi zinazowapatia fursa za kuitisha hongo. Mara nyingine, magenge ya uhalifu yanahonga polisi, maafisa wa uhamiaji na maafisa wa ushuru ili wapuuze uhalifu mipakani unaojumuisha ulanguzi wa madawa ya kulevya na silaha na unasaidia ukwepaji kodi

8. Mwanya baina ya sera na utekelezaji

Makundi anuwai ya kieneo barani Afrika, kwa mfano Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), yameunda sera ili kujaribu kuzidhibiti changamoto za usalama zinazokumbwa mipakani. Hizi zinajumuisha sera zinazohusu kuzuia, kudhibiti na kusuluhisha migogoro na mbinu za pamoja za kuzuia usafirishaji wa bidhaa haramu. Juhudi hizi zinalenga kuimarisha udhibiti wa mipaka, uhamiaji, na vita dhidi ya ugaidi. Kumekuwa na miito ya uratibu na uoanishaji wa mawakala husika ya nchi zilizoko kwenye makundi haya ili kupunguza vitisho vinavyotoka mipakani. Hata hivyo, miitiko ya serikali kwenye utekelezaji wa matakwa haya hayakuwa sawa kwa ajili ya sababu anuwai, sababu muhimu kati ya hizo ni ukosefu wa rasilimali na ukosefu wa ari ya kisiasa. Hii imesababisha mwanya baina ya sera na utekelezaji.

Huku sera hizi zinaashiria kujulikana kwa changamoto zilizoko, kwa ukweli, kiwango kidogo cha uwezo au rasilimali muhimu kimeundwa au kutengwa ili kuendesha sera hizi. Mawakala ya serikali kwenye vituo vya mipaka mara nyingi hawajapewa mafunzo vizuri na hawajui sheria zinazohusu masuala muhimu ya mipaka. Kwa ziada, serikali haijapatia kipaumbele maendeleo kwenye maeneo ya mipaka. Hii imeunda mazingira yanayowezesha mitandao ya wahalifu wa kimafia na wahusika wengine waliochanganyika na serikali wafanye shughuli zao.

Kwa ziada, maajenti wa kudhibiti mipaka wa nchi barani Afrika hawatarajiwi kutekeleza marufuku ya Umoja wa Mataifa ya silaha za Korea Kaskazini zinazonuiwa kufikia walinzi wa usalama au jeshi la nchi hiyo. Hii ni kwa ajili kukomesha usafirishaji wa bidhaa kama hizi kunapunguza usalama wa nchi wa nchi inayopokea bidhaa hizi. Kwa nchi nyingi, kushughulikia migogoro hii ya maslahi dhidi ya vikwazo vya Umoja wa Mataifa ni changamoto madhubuti ya sera na hakuna afisa wa ushuru anayetarajiwa kusuluhisha mtanziko huu.

9. Sera/taratibu dhaifu kwenye poti

Taratibu za ushuru kwenye poti za nchi nyingi barani Afrika zinaweza kuacha vipenyezo vingi vinavyoweza kutumiwa vibaya ili kukuza usafirishaji haramu. Kwa mfano, nchini Kenya, uthibitishaji au uchanganuzi wa 100% bado haufanyiwi mizigo yanayotolewa kauli kuwa yako njiani, mizigo yanayomilikiwa na wanaoshughulika kiuchumi ambao wamepewa idhini. Hii inamaanisha kuwa maafisa wa ushuru wanaruhusu mizigo ambayo hayajathibitishwa iingie nchini. Hii ni njia moja inayoweza kutumiwa kwenye ufichaji na ulanguzi wa haramu.

Enrico Carisch
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

www.comcapint.com
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025

Loraine Rickard-Martin
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

10. Uundaji wa hati bandia

Mawakala mengi ya mipaka barani Afrika hayana taratibu za kuthibitisha ikiwa hati za uhamiaji/uletaji nchini zinazonyeshwa kwenye vituo vya mipaka ni halisi. Mojawapo ya changamoto kubwa kabisa zinazokumba mawakala barani Afrika ni ankara bandia, kutaja bidhaa ambazo sizo, thamani ambazo sizo, maelezo ya anayesafirisha ambayo siyo, tarehe za miamala ambazo sizo n.k. Hati zingine zinazofanywa bandia zinajumuisha vyeti vya asili, orodha za upakiaji, na hati za uthibitishaji wa awali wa utiifu. Tatizo linazidishwa na ukosefu wa ushirikiano baina ya nchi. Hati bandia ni mojawapo ya njia zinazotumiwa kusafirisha bidhaa haramu/zisizoruhusiwa.

Kuhusu Thomas Bifwoli

	Thomas Bifwoli amefanya kazi na Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato Nchini Kenya (KRA); na aliidhinishwa awe Mkubwa wa Ofisi wa Ofisi ya Ushirikiano ya Upelelezi wa Kieneo ya Shirika la Ushuru Ulimwenguni ambayo ni ya Afrika Mashariki na Kusini (WCO RILO ESA). Alifanya kazi kama mratibu wa kundi la wataalamu wa ufuatilizi wa vikwazo vya Umoja wa Mataifa.

Nyongeza

Mifano ya maazimio na mapendekezo yanayotolewa na jumuiya za maeneo ya kiuchumi yanayolenga udhibiti bora zaidi wa mipaka ni:

- Mradi wa Kudhibiti Usambazaji wa SALW kwenye eneo la EAC, ulioanzishwa na Sekretarieti ya EAC pamoja na usaidizi wa GTZ (2006 –2009)
- Itifaki ya Nairobi ya Kuzuia, Kudhibiti na Kupunguza Bunduki Ndogo na Silaha Hafifu kwenye Eneo la Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika (2004)
- Kauli ya Dar-es-Salaam ya Kongamano la Kimataifa la Eneo la Maziwa Makuu (ICGLR) ya kuimarisha ushirikiano wa kieneo na ushirikiano baina ya nchi mbili kwenye nyanja za ulinzi na usalama (2004)
- Itifaki ya SADC ya Kudhibiti Silaha, Risasi na bidhaa zingine husika (2001)
- Mkataba wa Makubaliano wa Nanyuki wa Mikakati ya Kupambana na Ugaidi wa Kieneo (2006)
- Jitihada ya IGAD ya Upokonyaji Silaha wa Jamii za Wachungaji (Mei 2007)
- Maafikiano ya ICGLR ya Amani, Usalama na Utulivu wa Eneo la Maziwa Makuu (2006)

Enrico Carisch
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

www.comcapint.com
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025

Loraine Rickard-Martin
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com